# UFUGAJI WA KUKU

**Na Augustino Chengula**

## UTANGULIZI

Kuku yupo katika kundi la ndege wanaofugwa na binadmu, katika kundi hili la ndege wa kufugwa wapo pia bata, bata mzinga, bata bukini, njiwa, na kanga. Njiwa, bata na bata mzinga walianza kufugwa zaidi ya miaka 3,000 iliyopita nchini China. Kuku nao yasemekana walianza kufugwa miaka hiyohiyo wakitolewa katika misitu ya ndege ya Kiasia. Baaday ndege wakaanza kufugwa sehemu mabalimbali za bara la Marekani na Ulaya wakiwafuga kwa njia ya kienyeji. Mnamo karne ya 16 kuku waliingia Marekani wakitokea Ulaya na bata mzinga wakaingia Ulaya wakitokea Marekani.

Njia za kisasa za uanguaji wa mayai zilianza kutumika miaka ya 1870 lakini si kwa hatua ya kibiashara katika nchi za China na Misiri ya zama hizo. Ufugaji wa ndege kwa njia ya kisasa ulianza kutumika kuanzia karne ya 19 katika bara la Marekani na Ulaya wakilenga katika uboreshaji wa nyama na mayai. Tafiti na mbinu mbalimbali za ujengaji wa nyumba, ulishaji wa ndege, na uzalishaji wa kuku zilizoibuliwa zilipelekea kukua kwa kasi kwa ufugaji wa ndege na hasa kuanzia miaka ya 1930. Laikini ufugaji huu na ulaji wa ndege na mazao yake uliongezeka kwa kiasi kikubwa zaidi wakati wa vita kuu ya pili ya dunia kulipotokea uhaba wa nyama ya ng'ombe na nguruwe.

Nchini Tanzania haijulikani ni lini ufugaji wa ndege ulianza kufanyika, lakini huenda ulianza mara baada ya kuanza kuwa na makazi kutohamahama na hasa wakati wa utawala wa mkoloni. Kulingana na sensa ya mwaka 1994, idadi ya ndege iliyokuwa inafugwa wakati huo ilikuwa ni 29 685 220 na kati ya hawa kuku wa kienyeji walikuwa 20 163 811 na wa kisasa walikuwa 521 411 (wa nyama-368, 933 na wa

mayai-152 478). Ndege wengine wakiwa bata na bata bukini 743 472, bata mzinga 63 447, na kanga 37 942. Idadi hii imeongezeka sana kwa miaka ya karibuni kulingana na watu wengi kuvutiwa na ufugaji wa kuku na ndege wengine kwasababu ya faida zinazopatikana kwenye ufugaji wa ndege. Makadiro ya mwaka 2008 yalionyesha kuwa Tanzania ilikuwa na kuku milioni 36 na kati ya hao asilimia 95 ni kuku wa kienyeji, waliobaki ni wa kisasa.

**FAIDA ZA UFUGAJI WA KUKU**

Ukimtaja kuku katika maisha ya Mtanzania hakuna asiyemfahamu ama kwa kumuona au kwa kumla na hivyo kufanya kuwa kitu muhimu sana katika maisha ya kila siku. Asilimia kubwa ya Watanzania wanafuga kuku tena kuku wa kienyeji au kwa jina jingine kuku wa kijijini kwa vile asilimia kubwa (80%) ya wafugaji wa kuku wa kienyeji wapo vijijini. Kwa udogo wake, kuku amekuwa ndo mnyama rahisi wa kuchinja kwa kitoweo nyumbani, wajapo ndugu, jamaa na marafiki kutembelea familia. Hivyo kuku hawa wanafugwa kwa malengo makuu mawili; kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya nyumbani na kwa ajili ya kuongeza kipato katika familia. Kuku anafaida zifuatazo;

1. Kutumika kwa chakula na hivyo kupunguza tatizo la upatikanji wa protini katika familia
2. Kusaidia kuongeza kipato katika jamii na kusaidia kutatua matatizo kwa haraka zaidi maana uuzaji wake ni rahisi.
3. Kuku (jogoo) wamekuwa wakitumika tangu enzi kama saa ya familia wakati wanapotaka kuamka usiku kwa shughuli mbalimbali

Kuku ni mkombozi wa watu wenye kipato cha chini na watu wengi wanapenda kufuga kuku kwa sababu zifuatazo;

1. Watu wengi hasa mijini wanapenda kula nyama ya kuku na mayai hasa kuku wa kienyeji

2. Uwekezaji wa ufugaji wa kuku ni mdogo na hivyo kufanya watu wengei waweze kufuga kuku

3. Upatikanaji wa chakula cha kuku ni rahisi

4. Kuku wanahitaji muda mfupi sana kukua na hivyo faida yake inaonekana mapema

5. Urahisi wa upatikanaji wa dawa na chanjo

5. Gharama za matunzo ni ndogo na hasa kuku wa kienyeji

**KUANZA KUFUGA KUKU**

Ufugaji wa kuku chinin Tanzania upo wa aina kuu mbili, ufugaji wa kuku wa kienyeji na ufugaji wa kuku wa kisasa. Na kama tulivyokwisha kuona hapo juu ufugaji wa kuku wa kienyeji ndiyo wenye watu wengi zaidi na hii ni kutokana na ufugaji huo kuwa rahisi na usio na gharama kubwa.

Kabla ya kuanza ufugaji wa kuku (aina yeyote ile) kuna mambo ya msingi ya kuzingatia ili ufugaji wako uwe endelevu na wenye kukuletea manufaa makubwa na faaida zilizoainishwa hapo juu. Mtu yeyote anayetaka kufuga kuku lazima awe na dhamira ya dhati ya kutaka kufuga kuku maana kwa njia hii atawafuatilia kwa ukaribu na kuwapa mahitaji ya msingi ili waweze kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Anapaswa akae chini na kupanga kabla ya kuanza ufugaji wake, sehemu hii ya awali ya muhimu na haipaswi kurukwa na tena anayetaka kufuga kuku  ni vema akapata ushauri toka kwa wataalamu wa mifugo au wafugaji wengine wenye uzoefu.

Anatakiwa ajue ni aina gani ya ufugaji anataka kufanya (wa kuku wa kienyeji au wa kisasa), kuku wa nyama au wa mayai. Yote haya yatategemea na mahitaji ya eneo

alipo pamoja na mambo manne ya msingi ya mtaji, shamba/eneo la kufugia, usimamizi na masoko.

**KUKU WA KIENYEJI**

Ufugaji wa kuku wa kienyeji hasa kwa nchi yetu ndiyo unaongoza kwa kuwa na wafugaji wengi na wengi wapo kijini. Sababu kubwa ni kwamba ndio ufugaji rahisi na unaohitaji mtaji mdogo kuanzisha na kuku huvumilia sana magonjwa na adha nyingine za kimazingira. Ufugaji wa kuku wa kienyeji unasaidia kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kibiashara kwa familia masikini za vijini. Mbali na kwamaba kuku hawa wa kienyeji hutumiwa kama kitoweo mara kwa mara katika jamii, lakini pia kuku hawa huuzwa kuongeza kipato kinachosaidia familia kununua chakula madawa, nguo, kulipia kalo za shule kwa wanafunzi, pembejeo za kilimo, kutoa mahali, kwenye matibanu ya asili pamoja na mambo mengine ya kimila. Ufugaji wa kuku vijijini umeonekana kuwa njia mbadala ya kuongeza kipato na kusaidia kutatua matatizo ya wanancho hasa wakati ambapo mazao yao hayako tayari kwa kuyauza kutokana na kutokomaa au bei kuwa chini.

Kwa vile asilimia kubwa ya wafugaji wa kuku wa kienyeji wapo kijijini nitajikita zaidi kuelezea ufugaji wa vijijini kwa vile ule wa mijini unakaribiana sana na ule wa kisasa.

Kuna aina mbalimbali za kuku wa kienyeji wanaofugwa Tanzania na wafugaji wa wadogo. aina hizi zinatofautiana kwa umbo, uwezo wa kutaga na kuangua mayai, idai ya mayai wanayotaga na utunzaji wa watoto. Majina na aina ya kuku wanatofautina kulingana na eneo walikoanza kufugwa. Kuku wa kienyeji hutaga kwa wastani mayai 8-15 na aslimia 80 ya mayai yaliyoatamiwa huanguliwa. Kuku wa

kienyeji hutaga mara 2-3 kwa kila mwaka. Wafuatao ni baadhi ya aina ya kuku wa kienyeji waliokwisha tambuliwa na sifa zao:

**Kuchi au Kuza**- Hawa wana midomo mifupi na manyoya machache, wazitona wenye nyama nzuri, hutaga mayai machache 7-10 lakini huyaangua yote, utagaji wao ni kila baada ya miezi 4, wanapendwa sana na watu kwasababu ya ukubwa na uzito wao.

**Poni au Kishingo-**Umbo dogo, uzito mdogo, manyoya mengi, hutaga mayai hadi 20 na kuyaangua yote, utagaji wao ni kila baada ya miezi 4, ni walezi wazuri wa watoto.

**Mbuni-** Wana ukubwa wa kati, hawana mkia, hutaga mayai hadi 15 na huyaangua yote, utagaji wao ni kila baada ya miezi 3-4, hupata magonjwa kirahisi.

**Tongwe au msumbiji-** Hawa ni wafupi, thabiti, wenye umbo dogo na uzito mdogo, hutaga mayai hadi 20 na kuyaangua yote, utagaji wao ni kila baada ya miezi 3-4, walezi wazuri wa watoto, wanapendwa sana na wafugaji lakini si wanunuzi kwasababu ya umbo dogo.

**1.Mtaji**

Ufugaji wa kijijini unafanywa kwa kuwaacha kuku watafute chakula wenyewe wakitembea huku na kule kuokoteza chakula au mizoga. Hii inafanya gharama ya ufugaji kuwa ndogo, mtaji mdogo na ufugaji wenyewe kusimamiwa na mama na watoto.

a) ***Nyumba ya kuku***

Mara nyingi kuku hawa huko vijijini wanalala nje au ndani ya nyumba wanamolala binadamu. Wengine wamekuwa wakiwalaza kuku kwenye kona ya nyumba wanamolala, wengine kuwatengea chumba kimojawapo ndani ya nyumba

wanamolala na baadhi kuwalaza kuku kwenye vihenge vya kienyeji au kwenye mabanda ya kuota mota na jikoni wanako pikia vyakula na wengine wachache huwalaza juu ya miti. Ni asilimia ndogo sana wanaodiriki kuwajengea mabanda kuku wao, tena hasa kwa wakati huu ambapo hamasa ya ufugaji imongezeka kwa kutambua thamani ya kuku wa kienyeji. Vifaa kwa ajili ya ujenzi vinapatikana kwa urahisi katika eneo husika, kama tofali, miti, udongo na majani ya kuuzekea nyumba au mabanda ya kuku. Katika mazingira ya ufugaji wa kijiji mara nyingi kuku wengi hulazimika kulala kwa kubanana na hewa pia huwa si ya kutosha kwa kuku.

Mijini nako wameona thamani ya ufugaji wa kuku na hasa wa kienyeji ni kutokana na kuongezeka kwa soko la kuku wa kienyeji kwa vile nyama yake haina kemikali nyingi. Hawa wanafuga kwa kuwajengea kuku mabanda yao nje ya nyumba wanamo lala.

b) **Chakula na Lishe**

Kuku wa kienyeji mara nyingi hujitafutia chakula wenyewe huko vijijini na mara chache wanaweza kupewa pumba za mahindi, mtama, alizeti, punje chache za mahindi au mabaki ya chakula. Kwa hiyo mlo wao wa kila siku wanaupata kwa kutafuta mizoga ya wadudu pamoja na kula majani. Protini wanaipata kwa kula wadudu kwenye majani, udongo na magome ya miti.

c) **Mwanga na joto**

Kuku wa kienyeji hawapewi mwanga wa joto na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa mradi huu wa ufugaji.

d) **Gharama za dawa na chanjo**

Wafugaji wa kuku wa kienyeji kwa muda mrefu wamekuwa hawatumii dawa na chanjo kupambana na magonjwa kwa vile kuku hawa wanavumilia sana magonjwa. Lakini kadri ufugaji ulivyozidi kuwa na thamani na watu kukaa karibu karibu, kuku wa

kienyeji wakaanza kupata baadhi ya magonjwa japo si kama wa kisasa. na ugonjwa wa kideli ndiyo unaoonyesha kuwa sumbua wafugaji wa kuku wa kienyeji. Uzuri ni kwamba ugonjwa huu unachanjo na hivyo taratibu za uchanjaji zikifuatwa huwa si tatizo. Magonjwa mengine ni kama tyhoidi ya kuku, koksidiosisi, na viroboto. Hata hivyo gharama za kupambana na haya magonjwa ni ndogo kwa hawapati mara kwa mara. Njia zinazotumika kuzuia na kupambana na magonjwa ya kuku vijijini ni pamoja na njia za asili (madawa asili), na njia za kisasa (chanjo).

**e) Matatizo mengine ya kuku wa kienyeji**

Ukiondoa magonjwa, ufugaji wa kuku wa kienyeji huko vijijini matatizo kama wizi, ndege wala kuku kama mwewe, upatikanaji mgumu wa wataalamu wa mfugo, uhaba wa chakula na shida ya masoko vinarudisha nyuma maendeleo ya wafugaji wa kuku.

**2. Masoko**

Hakuna soko lililotengwa maalumu kwa ajili ya kuuzia kuku wa kienyeji toka vijiji au huko huko vijijini. Hata hivyo kunaongezeko kubwa sana la ulaji wa nyama na mayai toka kuku wa kienyeji mijini japo linalopelekea wafanyabiashara toka mijini kwenda kufuata kuku na mayai ya kienyeji huko vijijini. Kulingana na ongezeko la uhitaji wa kuku wa kienyeji linaoendelea kila siku, soko la kuku wa kienyeji kwa sasa si tatizo, hata wanaofuga hawawezi kutosheleza hitaji la soko hili huria.

**3. Uboreshaji wa ufugaji wa kuku wa kienyeji**

Kulinga na ongezeko la uhitaji wa kuku wa kienyeji katika soko, ipo haja ya kufanya ufugaji wenye tija kwa kuufanyia maboresho kidogo katika maeneo ya nyumba wanamoishi kuku, chakula chao, matunzo kiafya, na kuingiza kuku wanaozaliana zaidi au kuongeza thamani ya kuku wa kienyeji kwa kuchanya na aina ya kisasa.

Uzuiaji wa magonjwa unaweza kupunguza vifo vya vifaranga hadi asilimia 30. Ulishaji wa chakula kizuri unasaidia ufanyaji kazi mzuri wa mwili kama ukuaji, utagaji mayai, na ubora wa nyama. Ili kukidhi mahitaji wa walaji zipo haja za kuyafanyia utafiti madawa ya asili yanayotumika kwa kuyaboresha ili yatumike na kupunguza matumizi ya kemikali.

**KUKU WA KISASA**

**1. Mtaji**

Mtaji unaohitajika kuanzisha ufugaji wa kuku utategemea kwa kiasi kukubwa na ukubwa wa shamba lako la kuku unalodhamilia kulianzisha. Ufugaji wa kuku unamhitaji yake ya mwanzo ya uwekezaji kwa ajili ya;

a) ***Ugharamikiaji wa vitu visivyohamishika***

-Hapa tunazungumzia vitu kama vifaa vya ujenzi wa banda na gharama za ujenzi, vifaa vya maji ya kunywa na chakula, vifaa kwa ajili ya mwanga na joto, maeneo ya kulala na kutagia mayai (kwa kuku wa mayai).

**Banda** la kuku linatakiwa liwe na hewa ya kutosha lisiloweka unyevu na ukubwa wake utategemea idadi ya kuku unaotarajia kuwafuga. Kila kuku anahitaji eneo la mraba la kuanzia futi 1.5 hadi 1.8 wastani wa eneo za mraba 1.6, hapa jumla ya eneo linalo hitajika litazidishwa na idadi ya kuku unaotarajia kuwafuga.

**Vifaa vya maji**- Kuku wanahiji maji yawepo kila wakati wawapo bandani, hivyo kabla ya kuanzisha ufugaji wa kuku hakikisha kwamba unauwezo wa kupata maji safi kwa ajili ya kuku kila siku. Kama unatarajia kufanya ufugaji mkubwa hakikisha una matanki ya kuhifadhia maji kuondokana na ukosefu wa maji. Ndani ya banda weka vifaa 4 vya kunyea maji kwa kila kuku 100 na ukubwa wa vifaa hivyo utaongezeka

kwa kadri kuku wanavyokua. Kama unatumia vifaa vinavyotoa maji vyenyewe mfano mabomba basi sehemu mbili zinatosha kuwanywesha kuku 100.

**Vifaa vya chakula**-Matrafu matatu kwa kila kuku 100 lazima yawekwe ndani ya banda ili kuku waweze kula chakula kwa uhuru na si kwa kugombaniana. Kama matrafu yakiwekwa kwa njia ya kuyaning'iniza, basi matrafu mawili kwa kila kuku 100 yanatosha kulisha kuku. Ukubwa wa matrafu utaongezeka kadri kuku wanavyokua.

**Vifaa vya joto na mwanga-** Joto kwa kuku ni muhimu sana hasa kuku wakiwa katika hatua ya vifaranga ambapo hawawezi kuhimili baridi. Vifaranga wakiachwa kwenye baridi wanaathirika haraka na kupoteza uhai wao, hivyo joto kwao ni muhimu hadi wafikapo zaidi ya mwezi mmoja ambapo huanza kutengeneza uwezo wa kukabiliana na baridi. Wafugaji wadogo na hasa wale walio maeneo yasiyo na umeme wanaweza kutumia majiko yaliyotengenezwa mahususi kwa utumiaji wa mkaa kuhakikisha vifaranga wanapata joto. Lakini kwa wale walioko maeneo yenye umeme watumie taa za umeme zenye uwezo wa kutoa mwanga na joto (balbu na siyo tubulaiti). Kwa wale wanaotumia mkaa, basi mwanga utolewe kwa njia ya taa za mafuta zinazo ning'inizwa kwa juu, lakini hakikisha zinatoa mwanga wa kutosha ndani ya banda. Aidha kwa maeneo yasiyo na uhakika wa umeme taa za mafuta ziwekwe ndani ya banda kwa tahadhari.

**Stoo-** stoo ni muhimu kuwepo katika shamba la kuku itakayotumika kuweka vifaa, chakula, pamoja na mayai yanaokusanywa wakiwa wameanza kutaga (kwa kuku wa mayai). Trafu ndo za chakula na maji vinaweza kutunzwa humo kwa msimu mwingine wa vifaranga.

b) ***Matumizi ya kawaida ya kila siku***

Haya ni matumizi ya kununua vifaranga, kulipia bili za maji na umeme (kununua mkaa, mafuta), na kununua chakula. Vifaranga wanaotakiwa ku nunuliwa ni wale

waliotoka ktotolewa (wenye umri wa siku moja) na hakikisha unawapata kutoka kwenye shamba lenye uhakika wa kupambana na magonjwa. Aina ya chakula kitategemea aina ya kuku unaowafuga (wanyama au wa mayai). Vifaranga huanza kula mapema mara baada ya kuzaliwa na huendelea kula kadri wanavyo kua bila kupunguza kwa muda wa miezi minne.

**Chakula cha kuku wa mayai (Layers mash)**

Chakula cha mwanzo kabisa cha kuku wa mayai vifaranga) huitwa "*chiki mashi"* na kinahitajika wapewe vifaranga hadi watakapofikisha umri wa wiki 8-9*.*Kiasi cha protini katika chakula cha kifaranga wa siku moja hadi wiki 8 ni asilimia 22-24.

Chakula kinachofuata ni cha kuku wanaokua na hujulikana kwa jina la "*growazi mashi*" na waanapewa kuku hadi wanapofikisha umri wa wiki 18. Kiasi cha protini katika chakula hiki wanachopewa kuku wa kuanzia wiki 8 hadi 18 ni asilimia 14.

Aina ya mwisho ya chakula cha kuku wa mayai ni cha wale wanaoanza na walikwishaanza kutaga mayai. Kuku huanza kutaga mayai wakiwa na umri wa wiki 18-20 na chakula cha kuku wanaotaga mayai hujulikana kwa jina la *"leyazi mashi"* na huwa na asilimia 16-20 ya protini.

**Chakula cha kuku wa nyama (Broiler's mash)**

Tofauti na kuku wa mayai wanaopewa chakula cha aina tatu, kuku wa nyama wao hupewa chakula cha aina mbili kama ifuatavyo;

Wakiwa na umri wa siku moja hadi wiki nne wanapewa chakula kinachoitwa "*chiki au broila stata"* chenye asilimia 22-24 ya protini kama ilivyo kwa vifaranga wa mayai.

Aina ya pili na ya mwisho wanapewa wanapokuwa kwenye umri wa wiki 5-7 ambapo uuzaji unaanza wanapewa chakula kinachoitwa broila finisha chenye asilimia 19-20 ya protini.

**Gharama nyingine**

Gharama nyingine za ufugaji wa kuku zitatokana na ununuzi wa chanjo pamoja na madawa ya kuwafanya kuku waendelee kuwa na afya na kuleta matunda ya kuridhisha kwa kukinga na kupambana na magonjwa ya kuku. Aina ya dawa na njanjo za kutumia unahitaji kupata ushauri kutoka kwa daktari wa mifugo aliyekaribu nawe. Pia matengenezo na marekebisho ya hapa na pale yatahitaji pesa pamoja na kuwalipa wafanyakazi wanao kusaidia kazi kwenye shamba lako la kuku. Lakini pia gharama nyingine za dharula zaweza kujitokeza, hivyo ni vema kuweka katika bajeti yako.

**2. Eneo la kufugia na uchaguzi**

Eneo la kufugia ni kitu muhinu sana cha kuzingatia wakati unapofanya uamuzi wa kutaka kufuga kuku. Wakati wa kuchagua eneo hilo vigezo vifuatavyo ni veme vikazingatiwa

i) Eneo liwe na nafasi ya kutosha tena ikiwezekana liwe kwenye mwinuko ili kurushu hewa ya kutosha.

ii) Eneo lisiwe karibu sana na makazi ya watu lakini kuweko na njia za mawasiliano hasa barabara ili kuruhusu uingizaji wa chakula na usafirishaji wa mayai na kuku kwenda sokoni.

iii) Eneo liwe na upatikanaji wa maji safi na umeme wa uhakika

iv) Eneo lisiwe na wadudu au wanyama waharibifu kwaa kuku au vifaranga

v) Epuka kuchanganya aina tofautitofauti za ndege kupunguza maambukizano ya magonjwa.

**3. Usimamizi katika ufugaji wa kuku**

Hii ni sehemu ya muhimu sana katika mradi wa ufugaji wa kuku kama ilivyo kwa mradi wowote kwani bila umakini katika usimamiaji mradi utakufa au hautaleta matunda yaliyotarajiwa. mambo ya msingi ya kusimamia ili ufugaji uwe na tija ni pamoja na chakula, udhibiti wa magonjwa, na udhibiti wa watu wanaoingia ndani ya shamba au banda lako. Chakula lazima kisimamiwe kwa uangalifu ili kupunguza upotevu lakini pia kuwa na hakika kuwa kuku wako wanapata chakula kinacho stahili na kwa wakati ili waweze kuku vema na kutaga mayai mengi. Kuku wapewe chakula nusu ya chombo wanachotumia na kisha nusu nyingine baadaye ili kuepuka wasije wakakimwaga kama tabia yao ilivyo, lakini pia kuku hula vizuri chakula kikiwa hakijakaa muda mrefu ndani ya chombo.

Kuku wa kisasa hushambuliwa na magonjwa mengi, lakini mengi yanatokana na uchafu ndani ya banda. Maambukizi haya yanaweza kutokana na vyombo vichafu vya maji ya kunywa, chakula chenye wadudu waliotokana na kunyesi cha kuku. Ili kuzuia kuku kunyea chakula ni vema kuning'iniza vyombo vya chakula ili kuku asiweze kupanda akiwa anakula chakula na kuchafua chakula. Unyevuunyevu ndani ya banda lazima uepukwe ili kupunguza maambukizi ya magonjwa ya mapafu na uzalianaji wa vimelea vya magonjwa.Baadhi ya magonjwa yanashambulia kuku ni pamoja na Koksidiosisi, ugonjwa wa Mareksi, Gumboro, Kideli, Taifodi ya kuku, ndui na minyoo. Ni vema kumtafuta daktari wa mifugo aliyekaribu nawe kwa ushauri wa na namna ya kukabiliana na magonjwa haya kwa kuku wako tena hata kabla ya kuanza ufugaji.

**4. Masoko**

Kazi ya kutafuta masoko inatakiwa kufanyika hata kabla ya wakati wa uuzaji wa kuku au mayai kufika. Tena ni vema kujiridhisha hata kabla ya kuanza kufuga kama

masoko yapo na ni wapi na utayafikiaje. Hii itakurahisishia wakati ukifika unakuwa hupati shida yeyote ile. Mambo yafuatayo lazima uyazingatie wakati unatafuta soko la kuku au mayai;

i) Biashara yako lazima iwe karibu na masoko ya kuku au lazima kuwe na urahisi wa kufika kwenye masoko ya kuku (yawepo mawasiliano ya barabara).

ii) Biashara ya aina gani unataka kufanya, mayai au kuku, wazima (hai) au waliochinjwa na kutengenezwa.

iii) Lazima ujue bei ya aina ya bidhaa kabla ya kuipeleka sokoni (siku hizi simu za mkononi zimerahisiha mawasiliano)

iv) Fanya matangazo ya biashara yako kabla ya kuanza kuuza ili watu wajue, tene ni vema ukaanza matangazo mapema kabisa ikurahisishie kupata masoko.

**5. Utunzaji wa kumbukumbu**

Mali bila daftari huisha bila kujua, ni vema kutunza kumbukumbu ya mambo yote ya muhimu yanayofanyika ndani ya shamba lako la mifugo. Mbali na kumbukumbu nyingine, mambo yafuatayo lazima yawekewe kumbukumbu; namba ya kuku ulionao kwa umri wao, kumbukumbu ya chakula, tarehe za matibau na chanjo, tarehe za kuja daktari wa mifugo, kumbukumbu za vifo, mayai yaliyotagwa, mauzo ya mayai au kuku, gharama za maji na umeme na gharama za wafanyakazi. Hii itasaidia kujua kama kuna faida au hasara inayotokana na ufugaji wako wa kuku. Hivy ni muhimu kufanya mahesabu ya mapato na matumizi kila baada ya muda fulani hasa kila mwaka ili ujue kama kuna hasara inatokana na nini uirekebishe.